**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA**

**Phone0713535202 Mkuu wa Shule**
**0656140560 M/Mkuu wa Shule**

**P.BOX 145,**
**KILOSA-MOROGORO.**
**TANZANIA.**
**Barua pepe: kilosa.secondary@kilosadc.go.tz**

---

**Kumb. Na: SSK/JI/F1/2026**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………………………………………………………….
S.L.P……………………

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026 KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO YA KILOSA ILIYOPO WILAYA YA KILOSA, MKOA WA MOROGORO**

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** mwaka **2026** katika shule hii. Shule ya Sekondari ya Kilimo Kilosa ipo umbali wa **KM 26** kutoka Halmashauri ya Wilaya Kilosa katika mkoa wa Morogoro. Kuna njia mbili za usafiri zitakazo kufikisha shule ya Sekondari ya Kilimo Kilosa.

Mosi, **usafiri wa Treni ya SGR (treni ya kati na mwendo kasi).** Tunashauri watakaoamua kutumia njia hii kutoka Dar es salaam,Morogoro Dodoma, Kigoma na mikoa ya kanda ya ziwa . Nenda stendi ya mabasi ya wilaya ya Kilosa, Panda gari zinazokwenda Dumila. Shuka kituo cha Rudewa (nauli ni tsh 3000 tu). Chukua bodaboda wakulete Kilosa sekondari (kizunguzi) na nauli ya bodaboda ni Tsh **2000** tu.

Pili, **usafiri wa mabasi** kwa watakaotumia njia inayopitia mkoa wa **DODOMA** washuke kituo cha Dumila. Ulizia stendi ya magari yanayo kwenda Kilosa, Panda gari hiyo inayoenda Kilosa halafu shuka kituo cha Rudewa (**nauli ni Tsh 4,000/=**). Chukua bodaboda hadi shuleni. Kwa watakao tumia njia inayo pitia Chalinze (Pwani) na mkoa wa Iringa, shuka kituo cha mabasi cha mkoa wa Morogoro **(MSAMVU).** Panda gari ya kilosa kupitia **Dumila** na shuka kituo cha Rudewa **(Nauli ni Tsh 8,000)**, panda bodaboda hadi shule na nauli ya boda boda ni **Tshs 2000**

**Muhula wa kwanza kwa mwaka wa masomo 2026 unaanza tarehe 13/01/2026. mwanao anatakiwa Kuripoti shuleni tarehe 11 /01/2026 na 12/11/2026 Mwisho wa kuripoti ni wiki moja baada ya tarehe ya kufungua.**

**Aidha S**hule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya **Elimu Na 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na 10** ya mwaka **1995**, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sanyansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

i. Aje na Suruali mbili za rangi ya damu ya mzee (**Redish Brown**) iwe na marinda mawili kulia na mawili kushoto isiwe ya kubana yaani “Model” upana chini usipungue sentimeta 16. kwa watakaoshindwa kushona nyumbani zinapatika karibu na eneo la shule kwa Shilingi Elfu ishirini **(20,000/=)** tu.

ii. Aje na Suruali mbili za kuvaa nje ya darasa rangi ya (**Dark Blue)** iwe na marinda mawili kulia na mawili kushoto isiwe ya kubana yaani “Model” upana chini usipungue sentimeta 16. Kwa watakaoshindwa kushona nyumbani zinapatikana karibu na eneo la shule kwa Shilingi Elfu ishirini **(20,000/=)** tu.

iii. Mashati ya shule mawili (2)

iv. Viatu vyeusi vya kufunika vya kamba. Viatu vya mtindo wa magorofa au mabuti haviruhusiwi

v. Soksi nyeusi pea mbili au Zaidi.

### 2.2. NGUO ZA ZIADA ZINAZORUHUSIWA SHULENI (MICHEZO NA KUSHINDIA)

a) Fulana ya ndani nyeupe mbili au Zaidi.
b) Leso (handkerchief) na Taulo.
**c)** Tshirts 2 za njano (maarufu form six) (zenye nembo ya shule) za kushindia. ***Zinapatikana karibu na eneo la shule kwa shilingi 12,000/=***
d) Sweta la bluu lenye shingo ya V.
e) Bukta ya rangi Blue Bahari na jezi yake inayo fanana rangi Blue bahari isiwe na maandishi yoyote
f) Viatu vya raba (canvas shoes) na viatu vya kuchezea mpira wa miguu.
g) Track suit ya blue bahari pia inapatikana karibu na eneo la shule kwa shilingi **25,000/-**
h) Mabuti ya mvua (Rain boots).
i) Nguo za ndani (Boxer) dazani 1 kwa ajili kuepuka maradhi ya ngozi katika maeneo ya siri.(zinaweza kununuliwa duka la shule

2.3 **SEHEMU YA KULALA (BWENINI) NA JIKONI.**

a) Godoro la upana wa futi 2½. Maeneo karibu na shule yanauzwa 45000/=
b) Shuka mbili (light blue/blue isiyokolea).
c) Blanketi moja.
d) Chandarua (ni lazima).
e) Tranka (sanduku la bati lenye kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake.)
f) Sahani, kikombe, bakuli (aina ya mfupa) na kijiko.Hata shuleni vinapatikani

**2.4 VIFAA VYA DARASANI.**

a) Mathematical set.
b) Rula
c) Kalamu za kutosha.
d) Daftari kubwa zisizopungua 11 (counter books Q3)
e) Rimu ya karatasi 1 kila muhula ***((A4) siyo za mistari***
f) Taa ya juu (solar) kwa ajili ya dharura ikiwa umeme utakatika.
g) Box file

**2.5 VIFAA VYA KILIMO NA USAFI BINAFSI WA MWANAFUNZI.**

Aje na vifaa vya usafi na kilimo.

a) Jembe na mpini wake 01
b) Brash gumu (Hard bloom) lenye mpini wake.
c) Sabuni ya chooni ya maji lita 5 (Original) kutoka kampuni halisi
d) Zibulio la chooni (planka).
e) Ndoo mbili (lita 10) na galoni ya lita 5 ya kutunzia maji ya kunywa.
f) Sabuni ya kufulia, kuogea na Mafuta ya kupaka mwili.
g) Skwiza (Squizer) 01
h) Panga 01
j) Fagio la chelewa
k) Vidonge vya choo.Vinapatikana eneo la shule.

Shule yetu ina Amali mbili (2) zisizo za kihandishi Amali hizo ni: **AFYA YA WANYAMA (ANIMAL HEALTH AND PRODUCTION)** NA **UZALISHAJI WA MAZAO (FIELD CROP PRODUCTION**

**VIFAA VYA AMALI**

i).Miwani ya usalama (Safety Glasses) – Vinapatikana maduka yaliyokaribu na eneo la shule
ii) .Maski ya mdomo na pua (Mouth na Nose Mask- Vinapatikana maduka yaliyokaribu na eneo la shule
iii).Leather Gloves-Vinapatikana maduka yaliyokaribu na eneo la shule
iv).Over Ralls ya Dark blue kwa wanafunzi wa amali ya afya ya mifugo (Animal Health) na Kijani kwa wanafunzi wa Uzalishaji wa mazao (Field crop Production) Vinapatikana maduka yaliyokaribu na eneo la shule.
V.Gloves ngumu

**ZINGATIA**

1. **Mitindo ya unyoaji aina ya kiduku na kipara hairuhusiwi shuleni.**
2. **Nguo za nyumbani haziruhusiwi shuleni, mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule.**
3. **Viatu aina ya jenje na "safari boot" haziruhusiwi shuleni.**

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

**S**hule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sanyansi na Teknolojia,yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

## 3.1 KANUNI ZA LAZIMA KUFUATWA NA WANAFUNZI WOTE SHULENI

a) Kula chakula cha shule ni lazima kulingana na ratiba iliyopo labda kama kuna ushauri wa kitaalamu unaoshauri vinginevyo. Shule ina balance diet ila haina special diet kwa wanafunzi.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ya ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule. Ikiwa na pamoja na;

   i. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
   ii. Kuwahi katika kila shughuli za shule.

c) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya mazingira ndani ya shule

d) Kutunza usafi wa mwili, Mavazi na Mazingira ya shule. Kuoga na kufua nguo za ndani ni lazima.

e) Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shule na wakati wa kusafiri kutoka na kurudi shuleni.

f) Kutunza Mali za Umma kwa uaminifu na kwa Uzalendo .

g) Heshima kwa viongozi ,Wazazi ,Wafanyakazi wote ,Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

h) Hairuhusiwi mwanafunzi kuwa na vitu vya thamani kubwa bwenini bila kibali cha mkuu wa shule, ikiwa na pamoja nakuwa pesa nyingi bwenini au darasani.

## 3.2) MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

a) Wizi

b) Kumiliki simu au laini ya simu au chaji ya simu.

c) Utoro ikiwa ni pamoja na kulala nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule au Kukosa kuhudhuria vipindi darasani au kutofanya mitihani na majaribio kwa makusudi au kwenda nje ya shule bila kibali.

d) Uasherati,Ushoga, Ulawiti na Ubakaji.

e) Ulevi na Matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine, mirungi,kubeli na kadhalika.

f) Kupigana au Kupiga.

g) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.

h) Kudharau bendera ya Taifa.

i) Kuoa au Kuolewa.

j) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na Usalama wa Shule au Watu.

k) Kukataa adhabu kwa makusudi uliyopewa na Mwalimu.

l) Kufanya au Jaribio la kuua au kujiua au kutishia kujiua au kuua mwezako.
m) Kushiriki matendo ya kiharifu yanayo pelekea kuvunja sheria za nchi.
n) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako au watu wengine.
o) Kuvuka mto Wami unaozunguka eneo la shule. Mto huu ni hatari una Mamba na Viboko.
p) Kufanya biashara ya kukopesha pesa kwa wanafunzi au mtu yoyote kwa riba au bila riba ndani ya eneo la shule.

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI WAKATI WA KURIPOTI.**

Kila mwanafunzi ahakikishe anajaza kwa umakini fomu zifuatazo kabla ya kuja shuleni aidha mzazi unatakiwa kuipakua fomu hii na kuinakilisha(print) kwa ajili kuisoma na kujaza sehemu zote zinazopaswa kujazwa.

Kama kunasehemu hujaelewa wasiliana na Mkuu wa shule au Makamu Mkuu wa Shule kupitia namba zilizopo ukurasa wa kwanza wa fomu hii.

Aidha fomu zifuatazo ni lazima ziletwe shuleni zikiwa zimejazwa kwa ukamilifu wake.

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0 HITIMISHO**

**Shule yetu ni shule ya kilimo hivyo mwanao anatakiwa awe tayari kushiriki na kupenda masuala yanayo husiana na kilimo, hata kama hasomi somo la kilimo.**

Hakikisha mzazi au mlezi umesoma kwa umakini fomu hii na kujadiliana na mwananao juu yauatayari wake katika kuzingatia yaliyo tajwa kwenye fomu hii.

Utunzaji wa mazingira na kushiriki shughuri zingine zenye kuhamasisha uzalendo kwa nchi yetu ni lazima ikiwemo kushiriki katika vikundi mbalimbali hapa shuleni mfano; MALI HAI CLUB, PCCB, FEMA, SCOUT n.k

Karibu sana,

…………………………………

Wenceslaus A.Kihongosi

**Mkuu wa Shule**

# SHULE YA SEKONDARI YA KILOSA

## FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

Bandika picha
hapa
(yenye shati jeupe)

**1. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

A. Jina kamili la mwanafunzi

i. JINA LA KWANZA..............................................................

ii. JINA LA BABA...................................................................

iii. JINA LA UKOO.........................................................................

B. Tarehe ya kuzaliwa..................................Mwezi............................Mwaka.........................

**(Ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa)**

C. Mahali alipozaliwa; Kijiji/Mtaa................................Kata ........................................

Wilaya...................................................... Mkoa...............................................

D. Mwanafunzi huyu ni YATIMA au SIYO YATIMA. ( kama ni yatima eleza uyatima wake ni mzazi mmoja au wazazi wote)

...........................................................................................................................................

...........................................................................................................................................

E. Taarifa za shule ya msingi uliyo Soma.

i. Jina la Shule

...........................................................................................................

ii. Prem Namba ya mwanafunzi...............................................................

(Taarifa hizi zinapatikana shule ya Sekondari uliyosoma zijazwe kwa usahihi)

F. Mawasiliano ya mwanafunzi.

i. Namba ya simu 1....................................................Mzazi/Mlezi

ii. Namba ya simu 2.....................................................Mzazi/Mlezi

iii. Namba ya simu 3.....................................................Jirani

iv. Namba ya simu 4...............................................Afisa Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa.

Jina, Saini na muhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa.

**2. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI**

a) Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………………………………………

b) Kazi ya mzazi/mlezi………………………………………………………………………………

c) Namba ya Kitambulisho cha Taifa ………………………………………………………

d) Anwani ya Mzazi/mlezi S.L.P.………………………………ENEO……………………………

e) Mtoto wangu ni MLEMAVU AU SIYO MLEMAVU (kama ni mlemavu taja aina ya Ulemavu wake).

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

f) Ndugu ninao waruhusu kumtembelea mtoto wangu akiwa hapo shuleni ni (ANDIKA JINA , MAWASILIANO NA UHUSIANO WAKE)

i. JINA ………………………………………uhusiano…………………………………simu ………………………

ii. JINA ………………………………………uhusiano…………………………………simu ………………………

iii. JINA ………………………………………uhusiano………………………………… simu………………………

iv. JINA ………………………………………uhusiano…………………………………simu ………………………

v. JINA ………………………………………uhusiano…………………………………simu………………………

# AHADI NA KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………………………………………………Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA KIDATO CHA 1** mwaka 2024 ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yaTaifa na Shule ya Sekondari ya Bweni Kilosa.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni:

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu.
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumuita mzazi/ mlezi wangu. ……………………………………………………… (Jina la mzazi) kwa ajili ya hatua zaidi.

Saini ya mwanafunzi………………………………………… tarehe …………………………………………………………………

---

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ………………………………………………………………….ninakubali mtoto wangu Kupata na kupokea nafasi katika shule ya Sekondari Kilosa mwaka 2023. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa. **Na ninaahidi kufuatilia maendeleo yake ya kitaaluma na tabia kila muhula bila kukosa.**

Anuani yangu ya kudumu ni ………………………………………………………………………………………………

Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Saini ya Mazazi/Mlezi …………………………………………Tarehe ………………………………………………………

**KILOSA AGRICULTURAL SECONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

***FROM:*** The Medical Officer, ***TO***: The Headmaster,

................................................... Kilosa Secondary School.

P. O. BOX 145

........................................ KILOSA

**RE: MEDICAL CERTIFICATE**
**(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

I have examined.......................................... who seeks to join Form III in your school as follows:

| **AREA** | **REMARKS** |
|---|---|
| 1. Skin | ................................................................................................ |
| 2. Eyes | ................................................................................................ |
| 3. Ears | ................................................................................................ |
| 4. Teeth | ................................................................................................ |
| 5. Chest | ................................................................................................ |
| 6. Spleen | ................................................................................................ |
| 7. Abdomen | ................................................................................................ |
| 8. Urine | ................................................................................................ |
| 9. Stool | ................................................................................................ |
| 10. HB Hemoglobin | ................................................................................................ |
| 11. Inoculation against meningitis | ................................................................................................ |
| 12. Sickle cell | ................................................................................................ |
| 13. Asthma | ................................................................................................ |
| 14. Any other comments | ................................................................................................ |
| 15. blood Group | ............................................................................................ |

I consider that he/she* is physically/not physically fit to join your school.

Signature..........................................
Date................................................
Official stamp.................................

**SARE ZA SHULE**

